




#DuniaMojaTu

Mwongozo wa Vitendo vya kuishi kwa uendelevu
kupatana na mazingira

Umetengenezwa kwa ajili ya Siku ya Mazingira Duniani
Mwaka wa 2022



Picha: Zhang Fengsheng/Unsplash



SIKU YA
MAZINGIRA
DUNIANI 2022




Sweden
Sverige

Yaliyomo

Utangulizi	3
Jiunge na kampeni ya #DuniaMojaTu ya Siku ya Mazingira Duniani Mwaka wa 2022	4
SOS ya Sayari	4
Mabadiliko chanya	5
Kufanya kuishi kwa uendelevu kuwa chaguo msingi	5
Nambari za Kushughulikia Dunia: Kufanikisha matendo yako!	6
Mwongozo wa vitendo vya Siku ya Mazingira Duniani	7
Serikali	8
Funga pengo la uzalishaji wa gesi chafu - sasa!	8
Kulinda na kuboresha mazingira	8
Safisha hewa na maji yetu	9
Miji na mamlaka za mitaa	10
Kushughulikia Tabianchi	10
Kushughulikia Mazingira	10
Kushughulikia Uchafuzi	10
Fedha	12
Uwekezaji	12
Benki ya biashara	12
Bima	12
Fedha za maendeleo	12

Biashara na viwanda	14
Nishati na tabianchi	14
Bidhaa na vifaa	14
Usafiri	15
Mifumo ya chakula	15
Mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kijamii na vikundi vya kidini	16
Chukua hatua ya kwanza	16
Ungana	16
Ongoza kwa njia inayoweza kuigwa	16
Sayansi na elimu	18
Fanya zaidi kupitia utafiti	18
Kuza waleta mabadiliko kupitia elimu	18
Ongoza kwa njia inayoweza kuigwa	18
Watu binafsi	20
Paza sauti	20
Fanya maamuzi endelevu	20
Pesa	20
Chakula	21
Vitu	21
Usafiri	21
Burudani	22



Utangulizi

Mabadiliko ya tabianchi, mazingira na uharibifu wa bayoanuai, uchafuzi wa mazingira na taka –ni ushahidi kwamba Dunia ipo katika "hali hatari" inayotuzunguka na na kuongezeka kila uchao. Wakati uo huo, mabilioni ya watu hawana mapato, chakula, makao, huduma za afya na elimu. Matatizo ya nishati na chakula baada ya janga la COVID-19 na kuongezeka kwa migogoro ulimwenguni kote ni sababu zaidi za kutufanya kuwa na wasiwasi.

Njia ya kutoka kwenye tatizo hili ni kubadilisha uchumi na jamii zetu ili kuzifanya ziwe jumuishi, za haki na zishikamane zaidi na mazingira. Ni lazima tuache kudhuru sayari na tuiboresha. Ni lazima tulinde tulichonacho na kurudisha kile tulichopoteza ili kuendeleza mustakabali bora na endelevu, ambapo kila mtu anaweza kustawi.

[Siku ya Mazingira Duniani Mwaka wa 2022](#) inaweza kusaidia kuharakisha mabadiliko haya. Kampeni ya mwaka huu, #DuniaMojaTu, inaangazia uhitaji wa kubadilisha uhusiano wetu na mazingira kupitia mabadiliko chanya kuhusu jinsi tunavyokula, kuishi, kufanya kazi na kusafiri.


Mwongozo huu unaonyesha hatua ambazo jamii, mashirika na watu kila mahali wanaweza kuchukua. Unaangazia wajibu mkuu wa serikali, miji, biashara, vikundi vya kidini na ufadhili ili kuwezesha maisha endelevu kwa kubadilisha matumizi, uzalishaji, miundombinu, uwekezaji na matumizi ya ardhi. Pia inajumuisha mifano ya maamuzi ya watu binafsi ya kuleta mabadiliko na kusukuma uchukwaji wa hatua.

Kuharakisha maendeleo kuelekea uendelevu ni muhimu. Katika hali nyingi, suluhu tayari zinapatikana, kwa bei nafuu na zinaweza kuongezeka. Bado tunaweza kuzuia hali mbaya zaidi ya tabianchi. Tunaweza kusitisha uharibifu zaidi wa bayoanuai. Tunaweza kulinda na kurejesha mifumo ya ikolojia iliyoharibika. Tunaweza kusafisha hewa yetu, maji na udongo. Tunaweza kurekebisha uhusiano wetu na mazingira, na bado tunaweza kufikia [Malengo ya Maendeleo Endelevu](#) (SDGs), yaliyokubaliwa mwaka wa 2015 na nchi zote za Umoja wa Mataifa. Lakini tunahitaji kuchukua hatua sasa.

Wanadamu waliungana hapo awali ili kuzuia majanga ya kimazingira, kurekebisha ozoni, kusaidia jamii zilizo hatarini, kuboresha mamilioni ya hekta za ardhi na mifumo ya ikolojia ya baharini inayolinda maelfu ya viumbe, na kupiga marufuku uchafuzi hatari – na kuokoa maisha ya viumbe wengi.

Acha ushindi huo uwe mwanga unaochochea hatua zaidi na kuangaza njia ya ulimwengu ambayo tunaweza kuishi kwa amani na mazingira.

**Ulimwenguni kuna mabilioni ya galaksi,
katika galaksi yetu kuna mabilioni ya sayari,
Lakini kuna #DuniaMojaTu.
Acheni tuitunze.**



Jiunge na kampeni ya #DuniaMojaTu ya Siku ya Mazingira Duniani Mwaka wa 2022

“Dunia Moja Tu” ilikuwa kauli mbiu ya [Kongamano la Stockholm mwaka wa 1972](#), ambao uliweka maendeleo endelevu kwenye ajenda ya kimataifa na kusababisha kuanzishwa kwa [Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa](#) na Siku ya Mazingira Duniani.

Miaka hamsini baadaye, utegemezi wetu kwa sayari hii nzuri ya samawati, na mikazo tunayoiweka, ni dhahiri zaidi kuliko hapo awali. Kupitisha [#DuniaMojaTu](#) kama kauli mbiu ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka wa 2022 kunasisitiza kwamba muda wa kupatanisha watu na mazingira unaisha.

Kampeni inaalika kila mtu kusherehekea Dunia yetu kupitia hatua ya pamoja za kushughulikia kipengele kimoja au zaidi cha dharura tatu ya sayari: mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa bayoanuai na mazingira, uchafuzi na taka. Zaidi ya kile ambacho watu binafsi wanaweza kufanya, serikali na biashara ziko katika nafasi nzuri zaidi ya kutumia nguvu na fedha zinazohitajika ili kuweka sera na miundomsingi kuwezesha maisha endelevu.

Vijana na vyama vya kiraia vina jukumu muhimu katika kutetea mabadiliko. Lakini vikundi vyote katika jamii vinaweza na lazima vichukue hatua kubadilisha jinsi tunavyotumia na kusimamia Dunia na rasilimali zake.

Siku ya Mazingira Duniani mwaka wa 2022 inakuja katika wakati muhimu. Tuko katika [Muongo wa Kuchukua Hatua](#) ili kutimiza SDGs,

[Muongo wa Umoja wa Mataifa wa Kuboresha Mifumo ya Ikolojia 2021-2030](#) unazidi kushika kasi, na maamuzi muhimu yatachukuliwa katika miezi ijayo kuhusu kutunza tabianchi na bayoanuai.

Tarehe muhimu kuhusiana na Siku ya Mazingira Duniani Mwaka wa 2022 zinajumuisha:

- **Aprili 20: Uzinduzi wa kampeni ya #DuniaMojaTu**
- **Mei 9–20: Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Jangwa COP15, Abijan, Côte d’Ivoire**
- **Mei 14: Siku ya Ndege Wanaohama Duniani**
- **Mei 22: Siku ya Kimataifa ya Bayoanuai**
- **Juni 2–3: Mkutano wa ngazi ya juu wa Stockholm+50, Stockholm, Uswidi**
- **Juni 5: Siku ya Mazingira Duniani Mwaka wa 2022**
- **Juni 8: Siku ya Bahari Duniani Mwaka wa 2022**
- **Juni 6–17: COP Basel, Rotterdam na Stockholm Mikataba ya Geneva, Uswisi**
- **Agosti 9: Siku ya Kimataifa ya Watu wa Kiasili**
- **Agosti 12: Siku ya Kimataifa ya Vijana**
- **Agosti 29 – Septemba 13: Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Bayoanuai, Kunming, China**
- **Septemba 13–27, 2022: Kikao cha 77 cha Baraza la Umoja wa Mataifa**

- **Novemba 7–18 2022: Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 27), Sharm El-Sheikh, Misri**
- **Desemba 10: Siku ya Haki za Kibinadamu**

SOS ya Sayari

Dunia inakabiliwa na dharura tatu ya kisayari: joto linaongezeka haraka sana kwa watu na mazingira kustahimili; kupoteza kwa makazi na shinikizo zingine kunamaanisha kuwa takriban spishi milioni 1 ziko katika hatari ya kutoweka; na uchafuzi wa mazingira unaendelea kutia sumu katika hewa, ardhi na maji yetu.

- Kiwango cha joto duniani tayari imeongezeka kwa [takriban Inyuzi joto](#) tangu nyakati za kabla ya viwanda, kukiwa na ongezeko kubwa zaidi kwenye ardhi. Matokeo yake, misimu inabadilika na dhoruba zinaongezeka; mafuriko, ukame, mawimbi ya joto na mioto ya nyika zinafanyika mara kwa mara na kusababisha uharibifu mkubwa
- Majanga ya tabianchi yanaongeza [shinikizo kwenye mazingira](#), huku viumbe na mifumo ya ikolojia inatatizika kustahimili. Makazi muhimu kuanzia kwa misitu ya mvua hadi kwa maeneo oevu yanaendelea kupotea kwa sababu ya upanuzi wa binadamu, ikiwa ni pamoja na ukataji miti ili kuandaa nafasi ya kilimo. Ukataji miti, uvuvi kupita kiasi na biashara haramu ya wanyamapori huangamiza idadi kubwa ya mimea na wanyama adimu.
- Uchafuzi wa hewa, mwingi kutokana na kuchoma fueli ya visukuku, husababisha vifo vya mapema karibu [milioni 7](#) kwa mwaka.

Virutubishi kutoka kwa kilimo, mchanga kutoka kwa mmomonyoko wa udongo na taka za plastiki zilizotupwa zinachafua maji safi na ya pwani

Sayansi inaonyesha kwamba majanga haya yanayohusiana ni matokeo ya matumizi yetu yasiyo endelevu ya rasilimali za sayari na utupaji wetu wa taka bila kuwajibika. Mahitaji yetu ya rasilimali yanashinda uwezo wa Dunia kuyakidhi kwa [wastani wa asilimia 75](#); watu huathiri kwa kiasi kikubwa karibu [robo tatu ya ardhi isiyo na barafu](#) na theluthi mbili ya bahari; na uzalishaji wa gesi ya ukaa lazima [upunguzwe kwa nusu katika miaka minane ijayo](#) ili kuweka ongezeko la joto duniani chini ya nyuzi joto¹⁵. Kuna ushahidi mpya kwamba {Familia>21 zinahusishwa na thuluthi mbili ya uzalishaji wa gesi ya ukaa, na [ripoti ya IPCC](#) ya hivi karibuni inaonyesha kwamba mitindo na tabia endelevu zinaweza kupunguza uzalishaji wetu kwa asilimia 40-70 kufikia mwaka wa 2050.

Mabadiliko chanya

Kukabiliana na changamoto za Dunia zinazohusiana kimazingira na kijamii kunahitaji suluhisho kamili. Vitendo vya hatua kwa hatua vimeshindwa kuzuia matatizo, na mabadiliko ya kimfumo, ya mageuzi yanahitajika ili kushughulikia wito wa msaada wa Dunia.

Habari njema ni kwamba suluhu na teknolojia zipo na zinazidi kuwa nafuu.

Kama ilivyobainishwa katika [ripoti muhimu ya UNEP](#), mabadiliko chanya yanahusisha mabadiliko katika mitazamo na maadili ya ulimwengu pamoja na mifumo ya kiteknolojia, kiuchumi na kijamii ya jamii zetu. Inahusisha uvumbuzi, kujifunza na ushirikiano, na urekebishaji wa miundo ya utawala, sera, miundo ya biashara, teknolojia na mifumo mbalimbali ya maarifa. Inahitaji upangaji wa sekta mtambuka na mbinu jumuishi ili kupata ushirikiano na

kushughulikia maeneo hatari yakiwemo chakula, usafiri, ujenzi, maji, nishati, mifumo ya ikolojia na afya ya binadamu.

Kufanya maisha endelevu kuwa chaguo msingi

Chaguo za kuleta mageuzi chanya yanahitaji kupatikana, kwa bei nafuu na kuvutia watu binafsi ili waweze kufanya maamuzi bora ya kila siku. Nyingi za chaguo hizi zinaweza tu kuundwa na taasisi kubwa zaidi: serikali ndogo na za kitaifa, taasisi za fedha, biashara, mashirika ya kimataifa na mashirika mengine yenye uwezo wa kuandika upya sheria, kuweka matarajio yetu na kufungua upeo mpya.

Kwa Siku ya Mazingira Duniani mwaka wa 2022, mashirika haya yanahimizwa kuwa mawakala wa mabadiliko chanya. Yale ambao tayari yamejitolea yanaweza kuanzisha sera mpya, mipango mipya na uwekezaji mpya. Pale ambapo mabadiliko yameanza, yanaweza kuharakishwa na kuimarishwa.

Watu binafsi na wanaohusika na asasi za kiraia ni watetezi muhimu, wahamasishaji na waungaji mkono. Kadiri tunavyopaza sauti zetu zaidi, kuisitiza kile kinachopaswa kufanywa na kuonyesha ni nani anayehusika, ndivyo mabadiliko ya haraka yatakavyopatikana. Utetezi wenye mafanikio pia unahusisha uwajibikaji - kwa kutoa wito kwa wahusika ambao wanafanya polepole sana au hawaishi kulingana na ahadi zao.

Pamoja na nishati, mifumo ya uzalishaji na utunzaji wa bayoanuai, maeneo muhimu yanayohitaji mabadiliko ni pamoja na biashara ya kimataifa na mifumo ya usafiri, jinsi tunavyojenga na kuishi katika nyumba zetu, miji na maeneo ya kazi na ibada, jinsi na wapi pesa zetu zinawekezwa, mifumo ya chakula, na kile tunachofanya ili kujiburudisha.

Kufanya kazi ajenda hii yenye kutia moyo tayari kumeanza na inashika kasi. Kwa kuunga mkono Siku ya Mazingira Duniani mwaka wa 2022 na kampeni ya #DuniaMojaTu na kuzingatia masuluhisho kama yale yaliyoainishwa hapa chini, unaweza kusaidia kuhakikisha kwamba sayari hii ya kipekee na maridadi inasalia kuwa makao mazuri kwa wanadamu.



Shiriki hatua yako ya #DuniaMojaTu ya #SikuyaMazingiraDuniani!

Mada ya [Siku ya Mazingira Duniani](#) ni "DuniaMojaTu," na tunataka kuonyesha wimbi la hatua ya kuleta mabadiliko ambalo tayari linaendelea kulinda na kuboresha makao yetu ya pamoja.

Tunawaomba watu na mashirika kote ulimwenguni kutumia nambari kuangazia shughuli zao, na kuzichapisha kwenye chaneli zao za mitandao ya kijamii na kushiriki kwenye ramani yetu ya dunia ili kuwatia moyo wengine kuchukua hatua kwa manufaa ya watu na sayari.

Kushiriki kwa kutumia "Nambari za Kushughulikia Dunia" ni rahisi, hivi ndivyo unavyoweza kujiunga kupitia hatua 3 rahisi.

1

Amua kitendo unachotaka kushiriki na uandike chapisho lako kama pointi mbili ambazo kila moja huanza na nambari.

Hapa kuna mifano michache:

Mfano A:

2 ni Dola milioni za fedha za malipo ya uzeeni ambazo hazikuwekezwa kwa fueli ya visikuku.

1 ni kampuni .

Mfano B:

60 ni idadi ya magunia ya taka zilizokusanywa.

30 Ni idadi ya wanafunzi wa shule ya msingi wanaosafisha mto wetu.

Mfano C:

5 ni idadi ya watu katika familia yetu.

1 ni idadi ya watoa nishati jadidifu anayeivezesha

2

Tusaidie kuweka hatua yako kwenye ramani ya dunia!

Enda kwenye <https://action.worldenvironmentday.global/>, andika kitendo chako na pata kadi ya mitandao ya kijamii inayoweza kupakuliwa unayoweza kushiriki na wafuasi wako.

3

Piga picha au rekodi video fupi inayoonyesha jinsi unavyoshughulikia dunia. Toa wasilisho lako kwa ubunifu! Kisha lichapishe kwenye chaneli zako za mitandao ya kijamii. Jumuisha Nambari zako mbili za Kushughukia Dunia, na uongeze #DuniaMojaTu na #SikuyaMazingiraDuniani kwenye mstari wa mwisho, hivi:

1,235 kWh ni kiwango cha nishati ya jua.

10 ni idadi ya mabasi ya umeme katika jiji letu.

#DuniaMojaTu #SikuyaMazingiraDuniani

Hakikisha umetaja @UNEP, kwa kuwa tutafuatilia michango ya jamii kwenye chaneli zetu za kidijitali.

Mwongozo wa Shughuli za Siku ya Mazingira Duniani

Kila mtu kila mahali anaweza kusaidia kuunda sayari endelevu zaidi. Katika kurasa zifuatazo kuna baadhi ya hatua ambazo mashirika na watu wanaweza kuchukua. Tafuta kiwango (au viwango) ambapo unaweza kufaidika zaidi, pata msukumo kutoka kwa mapendekezo haya na ujue jinsi unavyoweza kuwa na athari kubwa zaidi.

Shiriki hatua yako kwa kutumia Nambari za Kushughulikia Dunia, na kutumia **#DuniaMojaTu** na **#SikuyaMazingiraDuniani** kwenye mitandao ya kijamii.



Serikali

Ni serikali pekee zinazoweza kutekeleza mabadiliko ya mageuzi ya sekta mtambuka kwa kiwango kikubwa. Iwe katika ngazi ya kimataifa, kitaifa au kikanda, serikali ni kichochezi muhimu cha uendeleu. Sera kabambe na thabiti na utekelezaji wake endelevu na viongozi waliojitolea ni muhimu.

Pamoja na kudhibiti na kuweka mfumo wa fedha kwa ajili ya shughuli za binadamu, na kutekeleza sera zinazoshughulikia mazingira; jinsi serikali zinavyotumia fedha za umma – kuandaa ofisi au kuandaa usafiri wa wafanyakazi, kwa mfano – hutengeneza uhitaji katika soko na kuweka mifano.

Siku ya Mazingira Duniani ni jukwaa bora kwa viongozi na serikali kila mahali kuongeza juhudi katika ahadi zao za uendeleu na kubadilisha shughuli zao wenyewe na kutekeleza sera ambazo zitawezesha kila mtu kutatua majanga matatu ya sayari.

Hapa kuna baadhi ya maeneo muhimu ya kushughulikiwa, kadhaa kati yazo huleta manufaa katika dharura hizo tatu:

Punguza uzalishaji wa gesi chafu - sasa!

Ili kuepuka janga la tabianchi, uzalishaji wa gesi ya ukaa unahitaji kupungua kwa asilimia 45 kufikia mwaka wa 2030 na kukomeshwa kufikia mwaka wa 2050. Inaweza kufanyika ikiwa serikali zote zitaongeza juhudi kwa ahadi zao chini ya [Mkataba wa Paris](#) na kuchukua hatua madhubuti sasa kupunguza uzalishaji wa gesi chafu.

- Kuongoza kutoka juu. Fanya shughuli za kila siku za mashirika yote ya serikali zisiwe na kaboni kufikia mwaka wa 2030.

- Jisajili kufadhili na kutekeleza sera za kitaifa ili kutimiza [Mkataba wa Paris](#).
- Kuondoa fueli ya visikuku na kukomesha ruzuku ya fueli ya visikuku.
- Anzisha sera zinazochochea nishati jadidifu na kukuza matumizi mazuri ya nishati.
- Toza kaboni. Kuongeza bei ya kaboni kutachochea viwanda kutengeneza bidhaa kwa njia inayojali mazingira, na Waunda bidhaa, na wajenzi kujenga kwa kutumia nishati vizuri.
- Wekeza katika miundombinu ya nishati jadidifu, matumizi mazuri ya nishati na miradi ya usafiri isiyochafua mazingira ili kuhakikisha uendeleu
- Kukuza na kutegemeza kilimo kinachozingatia tabianchi na endelevu.
- Komesha na kubadili ukataji miti.
- Hakikisha kwamba fedha zote za serikali – ikijumuisha malipo ya uzeeni, akiba na bima – zinawekezwa kwenye kwenye miradi endelevu na hazidhuru tabianchi, afya ya binadamu au mazingira.
- Tumia uwezo wa manunuzi kukuza maisha endelevu. Kwa mfano, andaa vyakula vyenye lishe bora tu vyenye kiwango cha chini cha kaboni kwenye maduka ya watumishi wa umma na kuwachochea wafanyikazi kutembea, kuendesha baiskeli na kutumia usafiri wa umma kuja kazini.

Viungo

<https://www.unep.org/resources/emissions-gap-report-2021>

<https://www.iea.org/reports/net-zero-by-2050>

<https://www.unep.org/explore-topics/transport>

Kutunza na Kuboresha Mazingira

Serikali zinahitaji kuchukua hatua madhubuti duniani na kitaifa ili kukomesha kuzorota kwa mazingira na kuboresha mifumo ya ikolojia ya nchi kavu na bahari. Malengo ya zamani hayakutimizwa, kwa hivyo malengo mapya lazima yaungwe mkono na mipango thabiti ya utekelezaji na usaidizi wa kifedha.

- Kuwa mstari mbele katika kukubaliana na kutekeleza [Mfumo wa Kimataifa wa Bioanuwai 2020](#) kabambe na jumuishi ili kukomesha na kukabiliana na uharibifu wa bayoanuai na kuhakikisha matumizi endelevu ya mazingira.
- Tangaza uungaji mkono wa [Muongo wa UN wa Kuboresha Mifumo ya Ikolojia 2021-2030](#) na uchukue hatua ya kurejesha [hekta bilioni 1 zilizoahidiwa kurejeshwa](#) duniani kote.
- [Rekebisha mfumo wako wote wa kitaifa wa uhasibu](#) ili kuweka mtaji asilia kama nguzo ya tathmini ya utajiri wa binadamu na ustawi, na kuzitumia kuongoza sera za kiuchumi.
- Zindua mageuzi ya miundo ya kodi na ruzuku ili uzalishaji endelevu utoe ajira na ustawi, na uharibifu wa mazingira haulipi tena.
- Fuatilia [Tangazo Tamko la Viongozi wa Glasgow kuhusu Matumizi ya Misititu na Ardhi](#) ili kutunza na kuboresha misitu.
- Shirikiana na jamii za mitaa, za kiasili na za kidini ili kuelewa jinsi ya kuimarisha utiifu wa sheria na sera zilizoundwa kutunza mifumo ya ikolojia.

Viungo

<https://www.decadeonrestoration.org/>

<https://www.unep.org/resources/making-peace-nature>

<https://www.unep.org/resources/inclusive-wealth-report-2018>

Safisha hewa na maji yetu

Uchafuzi wa hewa unaua mamilioni ya watu kabla ya wakati wao kila mwaka na kuchangia majanga ya tabianchi. Licha ya kupiga hatua katika baadhi ya maeneo, ubora wa hewa ndani na nje ya majengo bado ni duni katika maeneo mengi. Wakati huo huo, plastiki, kemikali na taka zinaendelea kutiririka ndani ya bahari zetu. Hizi huua viumbe wa baharini, huunda maeneo yasiyotegemeza uhai na kuingiza kwenye maji yetu mamilioni ya tani za chembe ndogo za plastiki, zinazohusishwa na [athari mbaya za afya ya binadamu](#) na athari zisizojulikana za muda mrefu kwa watu na mazingira.

Hatua za kushughulikia uchafuzi ambazo serikali zinaweza kuchukua:

- Kuunda makubaliano ya kimataifa ya kukomesha uchafuzi wa plastiki baada ya mataifa 175 kuunga mkono [wito wa mkataba mpya](#) katika Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa la mwaka wa 2022.
- Piga marufuku, zuia au utoze ushuru matumizi ya plastiki inayotumika mara moja kama vile mifuko ya plastiki, vifungashio, chupa na vyombo.
- Boresha mifumo ya udhibiti wa taka ili miundombinu ifaayo ipatikane kupokea taka na uhakikishe kuwa sehemu kubwa inaweza kutumika tena au kuchakatwa tena.
- Punguza uchafuzi hatari wa hewa kwa kutumia miongozo ya [WHO ya hivi karibuni ya ubora wa hewa](#) na ufuatilie kwa ukaribu na kuhimiza ridhaa.

- Kutegemeza maendeleo ya nishati jadidifu nafuu isiyochafua mazingira, ikijumuisha ya kupikia, kupasha joto na mwangaza.
- Zindua na utekeleze sera za usafiri zisizochafua mazingira, ili kuwezesha raia na bidhaa kusafiri katika miji na nchi zao bila kusababisha uchafuzi wa hewa.

Viungo

<https://www.unep.org/interactives/beat-plastic-pollution/>

<https://breathelife2030.org/>



Miji na mamlaka za mitaa

Zaidi ya nusu ya watu bilioni 8 duniani wanaishi mijini, na idadi hiyo inazidi kuongezeka. Miji na majiji mara nyingi hubeba shinikizo kubwa la majanga matatu ya sayari, na serikali za mitaa na za kikanda ziko mstari wa mbele katika kukabiliana na hali hii. Mamlaka zinazowajibika za manispaa na mitaa na viongozi wao wanachukua fursa hiyo kubuni makazi endelevu kimazingira na kijamii ya siku zijazo.

Baadhi ya mambo ambayo miji na mamlaka za mitaa zinaweza kufanya:

Kushughulikia Tabianchi

- Kuongoza kutoka juu. Fanya shughuli za kila siku za serikali za mitaa kutozalisha gesi ya ukaa kufikia mwaka wa 2030.
- Punguza uchafuzi kwa manufaa ya vizazi vijavyo na usaidie kufikia malengo ya [Mkatoba wa Paris](#) kwa kujenga miundombinu endelevu na mifumo ya nishati jadidifu katika jamii yako.
- Unda mifumo endelevu na bora ya usafiri wa umma pamoja na njia salama na bora kwa wanaotembea na wanaoendesha baiskeli ili kupunguza matumizi ya magari, muda wa kusafiri na msongamano.
- Kuhakikisha fedha zote za serikali za mitaa – ikijumuisha malipo ya uzeeni, akiba na bima – huwekezwa katika miradi endelevu ambayo haidhuru tabianchi, afya ya binadamu au mazingira.
- Weka misimbo ya ujenzi inayojali mazingira na kujumuisha vihami bora na uingizaji bora wa hewa, paneli bora za jua, pampu bora

za joto, sehemu za kuchaji gari na kadhalika – tengeneza njia kwa kukarabati majengo ya umma!

- Jiunge na [Race to Zero](#), kampeni ya kimataifa ya kutafuta msaada wa kutozalisha gesi chafu, vizuri, kwa uthabiti na kutumia rasilimali kutoka kwa miradi kama vile mpango wa UNEP wa UrbanShift, mtandao wa mameya wa C40 na ICLEI – Serikali za Mitaa kwa Uendelevu.

Viungo

<https://racetozero.unfccc.int/system/cities/>

<https://www.shiftcities.org/>

<https://iclei.org/en/Home.html>

Kushughulikia Mazingira

- Boresha mifumo ya ikolojia ya mijini na utumie mazingira kwa maendeleo endelevu katika maeneo kama vile ardhi oevu mijini na korido za kijani ili kutoa makazi kwa bayoanuai, kukabiliana na vitisho kama vile mawimbi ya joto na mafuriko, na kufanya miji iwezeshe maisha zaidi.
- Kutoa maji safi na usafi wa mazingira kwa wote ili kupunguza uchafuzi wa njia za maji na mifumo ya ikolojia ndani na nje ya maeneo ya mijini, na pia kuzuia magonjwa
- Jiunge na mradi wa [CitiesWithNature](#) na usajili ahadi na hatua mpya ili kulinda bayoanuai katika jiji lako au nafasi nyingine ya mjini.

- Rejeshwa wanyamapori na uboreshe nafasi za umma zilizopo na kutelekezwa kwa kupunguza ukataji na kuhimiza kumea upya kiasili ili miti, wadudu, ndege, vipepeo na hata mamalia warudi na kustawi katika miji.

Viungo

<https://citieswithnature.org/>

<https://naturvation.eu/atlas>

<https://cities4forests.com/>

Kushughulikia Uchafuzi

- Zindua na utegemeza mipango na jamii, sekta ya kibinafsi na wengine ili kupata utegemezo na kukubaliana na njia ya mabadiliko, na kuunganisha mifumo ya upangaji kufanya maono yako ya kuwa na miji endelevu kutimia.
- Kusanya, tenganisha na kutupa taka kwa usalama ili kutunza ardhi na maji huku ukihimiza upunguzaji na kutumia tena taka kwa raia na wafanyabiashara.
- Nasa gesi kutoka kwenye mapipa ya taka za kikaboni ili uitumie badala ya fueli ya kisukuku.
- Weka malengo ya upunguzaji wa haraka wa uzalishaji na uchafuzi wa taka za plastiki katika manispaa yako na uandae kampeni na hatua za kuzifanikisha

- Tenga maeneo yenye uzalishaji mdogo wa gesi chafu katika maeneo yenye watu wengi ili magari yasiyochafua mazingira tu na usafiri wa umma yaweze kutumia barabara hizo.
- Leta jiji lako kwenye [mtandao wa BreatheLife wa UNEP](https://breathelife2030.org/breathelife-cities/become-a-breathelife-city/) ili uweze kutafuta na kushiriki njia bora za kuboresha hewa mijini

Viungo

<https://breathelife2030.org/breathelife-cities/become-a-breathelife-city/>

<https://globalabc.org/resources/publications/decarbonizing-building-sector-10-key-measures>



Ufadhili

Kufikia uendeleu kunahitaji mabadiliko ya hali ya juu ya ufadhili. Kuhimiza sekta kuhamia rasilimali jadidifu, na kuondoa vichafuzi na gesi za ukaa kunaweza kupunguza shinikizo kwa mazingira. Uwekezaji lazima ufanywe kwenye shughuli zinazothamini mazingira na kuleta ustawi kwa wote bila kuharibu mazingira.

Mazingira thabiti na ya uwazi, mbinu za kijamii na utawala (ESG), uangalifu unaostahili na ufichuzi unaweza kuleta mabadiliko chanya huku ukilinda sekta ya fedha dhidi ya shutuma za kujifanya kutuna mazingira.

Kuanzia kwa kubuni taasisi za fedha na fedha za uwekezaji hadi kwa makampuni ya bima na benki za biashara, wawekezaji wa kila aina lazima wafadhili siku zijazo na kuondoa joto duniani!

Wahusika wote wa kifedha wanapaswa kuoanisha mikakati yao ya biashara na malengo ya uendeleu ya kimataifa na kitaifa, ikijumuisha SDGs, [Mkataba wa Paris](#) na Mfumo ujao wa Bayoanuai.

Hapa kuna njia maalum za kuleta mabadiliko:

Uwekezaji

- Jiunge na [Wawekezaji wa Kimataifa kwa Maendeleo Endelevu](#) na [Net-Zero Asset Owners Alliance](#).
- Tekeleza [Kanuni za Uwajibikaji zinazoungwa mkono na Umoja wa Mataifa za Uwekezaji](#).
- Weka tarehe inayolengwa ya kutozalisha gesi ya ukaa kwa

washirika wa kampuni yako na upendeleo dhamana katika kampuni zinazofuata viwango vya juu vya ESG.

- Onyesha ukataji miti, uharibifu wa udongo, uzalishaji wa taka na mazoea mengine yanayodhuru mifumo ya ikolojia inayohusishwa na uwekezaji wako.
- Kuhamasisha uwekezaji katika shughuli kama vile misitu endelevu na uvuvi ambao unarejesha mifumo ya ikolojia na kunufaisha watu na mazingira.
- Kupitisha sera na malengo yanayohamisha mtaji, uwekezaji na ufadhili kwa makampuni yanayotumia plastiki tena au vitu mbadala badala ya plastiki, au malisho endelevu.
- Hakikisha fedha zote za ndani ya shirika – ikijumuisha malipo ya uzeeni, akiba na bima – zinawekezwa katika miradi inayounga mkono mipango endelevu ambayo haidhuru hali ya hewa, afya ya binadamu au mazingira. Kutowekeza kwenye miradi inayoenda kinyume.
- Hakikisha majengo unayoishi yamewekewa vihami ili kuboresha matumizi ya nishati na kwamba watoa huduma za nishati wanatumia vifaa jadidifu.

Benki za kibiashara

- Inahitaji na kusaidia wakopaji kufikia viwango vya juu vya ESG na kutekeleza mipango ya biashara isiyochafua mazingira ambayo itaimarisha uthabiti wa shughuli zao.
- Weka na ufikie malengo ya kupunguza mfiduo wako kwa wakopaji wenye athari hasi katika maeneo yanayojumuisha Tabianchi, matumizi mazuri ya rasilimali, bayoanuai na uzalishaji wa taka.

- Chapisha uchanganuzi wa athari inayohusiana na ESG ya shughuli zako na ujumuishe uendeleu katika ripoti yako ya kawaida.

Bima

- Fanya masuala ya ESG kuwa kipengele muhimu wakati wa kutathmini na kudhibiti hatari na kuwasaidia wateja kutathmini, kufichua na kushughulikia masuala yao ya ESG.
- Fanya kazi na watunga sera ili kuboresha mifumo ya kisheria ya kupunguza na kudhibiti hatari zinazohusiana na ESG.
- Toa utaalumu wako kuhusu kudhibiti hatari na uhamisho, kwa mfano kwa mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali yanayounga mkono maendeleo endelevu.

Ufadhili wa maendeleo

- Toa fedha zaidi za muda mrefu, zenye riba nafuu kwa nchi zinazoendelea ili ziweze kujenga uwezo, huduma, miundombinu na mtaji wa watu unaohitajika kufikia SDGs.
- Tenga fedha zaidi za tabianchi kwa ustahimilivu na urekebishaji ili kutegemeza mifumo ya onyo ya mapema na miundombinu inayostahimili tabianchi na kilimo.
- Fadhili programu zaidi zinazojumuisha malengo ya tabianchi, bayoanuai na uchafuzi wa mazingira na kuwezesha maisha endelevu.
- Anzisha programu za msaada wa kifedha kwa biashara zinazoanza na biashara zingine zinazounda bidhaa na huduma bunifu na zisizochafua mazingira kwa bei nafuu.

- Jiunge na [Hazina ya Wabia Wengi](#) ya Muongo wa Umoja wa Mataifa wa Kuboresha Mifumo ya Ikolojia ili kufadhili harakati za kuboresha dunia.

Viungo

<https://www.unepfi.org/>

<https://www.unpri.org/>

<https://www.gisdalliance.org/>

<https://www.unepfi.org/net-zero-alliance/>

<https://www.un.org/sustainabledevelopment/financing-for-development/>



Biashara na viwanda

Biashara na viwanda vina uwezo wa kuunda uchumi unaoweza kukidhi mahitaji yetu kwa uendelevu. Tunahitaji uchumi unaotumia bidhaa tena na tena huku ukitumia malighafi chache na kuthamini uendelevu. Ingawa watungasheria na wateja hawawezi kuwezesha na kuongeza shinikizo la mabadiliko, viongozi wa biashara ndio wanaweza kuendesha mageuzi ya kiuchumi.

Kampuni zinazopuuza athari zao kwa mazingira hazitengi wateja tu na kuwafukuza wawekezaji. Hatimaye, wanaweza kuhatarisha kuwepo kwao. Kampuni ambazo hupuuza hatari za ESG na kushindwa kubuni miundo mipya na uendelevu ya biashara zitapitwa na wapinzani au biashara zinazoanza na kuleta mabadiliko.

Wanaoongoza kwa njia mpya na nafuu za kukidhi mahitaji yetu ya maisha endelevu watapata manufaa ya gharama ya chini ya nyenzo na hatari, kuongezeka kwa mauzo na kupata mtaji kutoka kwa wawekezaji wa biashara zisizochafua mazingira. Wanaweza pia kujua mbele kuhusu kanuni za kubana na kupanda kwa gharama za nishati ya visukuku.

Hapa kuna mapendekezo ya hatua kwa wafanyabiashara katika maeneo manne muhimu kwa Siku hii ya Mazingira Duniani.

Nishati na tabianchi

Viongozi wa biashara wanaweza kujiunga na Mpango wa UN wa

Kutunza Tabianchi na kuimarisha mchango wao katika kukomesha na kukabiliana na janga la tabianchi kupitia vitendo kama vile:

- Kubuni na kupitisha mkakati wa biashara isiyochafua mazingira ambayo inathamini uendelevu, kupunguza uchafuzi na athari zingine za mazingira, na kuweka biashara yako katika nafasi ya kustawi katika kipindi cha mabadiliko kuelekea uchumi endelevu.
- Hamisha akiba ya kampuni yako, mpango wa malipo ya uzeeni na uwekezaji wa fedha kwa sekta ambazo zinaunga uendelevu na hazidhuru tabianchi, afya ya binadamu au bayoanuai.
- Jiunge na [Race to Zero](#) - kampeni ya kimataifa inayotafuta uungwaji mkono kutoka kwa biashara, miji, maeneo na wawekezaji kwa ajili ya kujiimarisha vyema kwa udhabiti bila kuzalisha gesi chafu vizuri.
- Weka malengo ya kupunguza uchafuzi kwa biashara yako, fanya kazi ili kuboresha matumizi mazuri ya nishati na kupunguza kaboni katika shughuli, bidhaa na huduma zako, na uripoti maendeleo yako hadharani.
- Shirikiana na mamlaka za kitaifa, mashirika ya serikali na mashirika ya kiraia ili kuunda sera na hatua zinazosaidia biashara kuchangia katika kujenga uchumi unaotoa uchafuzi mdogo wa gesi ya ukaa na kustahimili tabianchi.
- Shirikiana na mashirika mengine ya biashara katika ngazi ya kitaifa, katika tasnia yako na pamoja na mifumo ya usambasaji ili kuweka maono mapya, kupitisha viwango, kupunguza hatari, kusaidia kukabiliana na hali na kuongeza fursa zinazohusiana na tabianchi.

- Kuwa bingwa wa biashara kwa kuchukua hatua za haraka na za kina za tabianchi, kufanya kazi na wenzako, wafanyikazi, wateja wawekezaji na umma kwa jumla.

Bidhaa na vifaa

- Kubadilisha mifumo ya uzalishaji kutoka kwa muundo wa "kuchukua, kutengeneza na kutupa" hadi kwa uchumi unaotumia bidhaa tena na tena ili kufanya maisha yetu kuwa endelevu. Msingi wake ni jinsi sisi tunavyobuni bidhaa na huduma ili kukidhi mahitaji yetu, na jinsi uzalishaji na matumizi yake hutumia malighafi na nishati. Haya hapa ni baadhi ya mabadiliko ambayo biashara zako zinaweza kuanzisha Siku hii ya Mazingira Duniani.
- Pitisha mkakati wa biashara isiyochafua mazingira ambayo inathamini uendelevu, kupunguza athari kwa mazingira, na kuweka biashara yako katika nafasi ya kustawi katika kipindi cha mabadiliko kuelekea uchumi endelevu:
- Buni miundo mipya ya biashara na matokeo ya bidhaa na huduma zinazoweza kukarabatiwa, bidhaa zinazoweza kuboreshwa na za kudumu kwa kutumia malighafi, pamoja na programu zinazokusanya, kutengeneza upya, kubadilishiwa matumizi au kutumika tena mwishowe.
- Wekeza katika teknolojia za kidijitali zinazoweza matumizi ya bidhaa tena na tena kwa mfano, kutambua na kufuatilia bidhaa, nyenzo na vipengele endelevu.
- Weka malengo ya matumizi ya bidhaa tena na tena kwa njia endelevu na kufichua kikamilifu juhudi zako ili kuzifanikisha.

- Kuunga mkono kampeni za kuendesha mabadiliko ya tabia ya watumiaji wa bidhaa duniani kote, ikiwa ni pamoja na kukuza matarajio endelevu kama vile kutengeneza bidhaa za kudumu, zilizokarabatiwa na kutumiwa tena mara kwa mara.
- Jiunge na makampuni mengine katika [Ahadi Mpya ya Kimataifa ya Uchumi wa Plastiki](#) na uweke malengo ya kukabiliana na uchafuzi wa plastiki katika chanzo chake.
- Komesha matumizi ya bidhaa za plastiki zisizo za lazima, zinazoweza kuepukika, na zenye kusababisha matatizo na kuanza kutumia vifaa, bidhaa na huduma mbadala.

Usafiri

Usafiri unaotumia fueli ya visukuku ni chanzo kikubwa cha uchafuzi wa gesi ya ukaa na uchafuzi wa mazingira. Kuhamia kwa usafiri na uchukuzi endelevu ni muhimu ili kuwa na jamii zenye afya bora na sayari safi.

Hapa ni baadhi ya mambo ambayo sayari inahitaji kutoka kwa sekta ya usafiri na biashara zenye mahitaji makubwa ya usafiri:

- Kuimarisha usafiri-kama-huduma, kama vile baiskeli- na kutumia magari pamoja, na kuunganishwa kwa vifaa vya mijini ambavyo vinapunguza uchafuzi, trafiki na athari za mazingira.
- Sera za usafiri za shirika zilizobadilishwa kabisa, ikijumuisha magari ya umeme na kuhimiza kushiriki gari, kuendesha baiskeli/ kutembea na kufanyia kazi nyumbani.
- Ukuzaji na/au uwekaji wa vitu vinavyoweza kushiriki chaji ya umeme na magari mapya ya umeme kwa aina zote za usafiri.
- Fueli yenye kaboni ya chini kwa usafiri wa masafa marefu na kazi nzito, ikijumuisha meli na ndege.
- Mabadiliko kuelekea matumizi jadidifu katika kutengeneza magari, kwa mfano kupitia vifaa vipya, kutengeneza sehemu upya,

miundo ya msimu na baada ya kumaliza kutumika ili kuhakikisha kuwa athari za magari yanayobadilishwa zinafuatiliwa hadi yatakapokoma kutumiwa.

- Teknolojia mpya zinazotumia mbinu ya kielektrostatiki kukusanya chembe za plastiki wakati magurudumu ya gari yanaisha.
- Ujenzi endelevu wa barabara kwa kutumia, kwa mfano, vifaa asili na jadidifu.

Viungo

<https://www.unglobalcompact.org/>

<https://www.unglobalcompact.org/take-action/action/climate>

<https://sciencebasedtargets.org/>

<https://www.wbcsd.org/Overview/About-us/Vision-2050-Time-to-Transform/Resources/Time-to-Transform-Executive-Summaries>

<https://www.resourcepanel.org/reports/re-defining-value-manufacturing-revolution>

<https://www.businessfornature.org/>

Mifumo ya chakula

Jinsi tunavyozalisha, kusindika na kusafirisha chakula ni kichocheo kikuu cha majanga ya tabianchi na tishio kubwa zaidi kwa bayoanuai. Hapa kuna hatua chache kati ya nyingi ambazo biashara zinaweza kutangaza Siku ya Mazingira Duniani ili kubadilisha mifumo yetu ya chakula na kuwezesha watu kufanya chaguo endelevu zaidi:

- Unda upya mifumo ya chakula na bidhaa zisizochafua mazingira sana zinazotoa nishati na virutubishi kutoka kwa makundi mbalimbali ya vyakula na iliyo na thamani ya juu ya lishe.
- Kuzalisha chakula katika mifumo endelevu ya kilimo na uvuvi zinazohifadhi na kurejesha tija ya ardhi yetu na bahari, kuzuia uchafuzi wa mazingira na kulinda bayoanuai.
- Msururu wa ugavi bila malipo na inayoweza isiyotegemea ukataji

miti au ubadilishaji wa makazi mengine asilia

- Kuunga mkono kampeni za kubadilisha chaguo za watumiaji kuelekea vyakula vyenye afya na endelevu na kupunguza upotevu wa chakula.
- Tanguliza vyakula ambavyo ni vya kikanda, vya msimu, vya mimea na vinavyokuzwa kwa kutumia kemikali chache.
- Punguza upakiaji na utumie tu vifaa ambavyo vinaweza kutumika tena au jadidifu.
- Unga mkono na utumie lebo za chakula zinazoaminika na zinazoonekana zinazowawezesha wateja kufanya chaguzi endelevu.

Viungo

<https://www.fao.org/3/i9900EN/i9900en.pdf>

https://www.unglobalcompact.org/docs/issues_doc/agriculture_and_food/soil-principles.pdf



Mashirika yasiyo ya serikali, mashirika ya kijamii na vikundi vya kidini

Mashirika ya kiraia yanaweza kuchochea na kukuza hatua ili kuunda sayari endelevu zaidi. Siku hii ya Mazingira Duniani, una jukumu muhimu la kukumbusha serikali, wafanyabiashara na wahusika wengine wajibu na ahadi zao za kuunda maisha bora ya baadaye, na kuwawajibisha.

Hapa kuna baadhi ya mifano ya mambo muhimu ambayo shirika lako au kikundi cha kidini kinaweza kufanya:

Chukua hatua

Tambua na uchague masuala ya kimazingira ambayo yana athari na ni muhimu kwa kikundi chako, kama vile janga la tabianchi, uharibifu wa mifumo ya ikolojia, uharibifu wa bayoanuai au uchafuzi wa mazingira, na uzingatie hatua unazoweza kuchukua – kupitia mradi au kutoa wito wa kuleta mabadiliko. Kwa mfano, unaweza:

- Zindua au usaidie mradi wa kuboresha mazingira chini ya Muongo wa Umoja wa Mataifa wa Kuboresha Mifumo ya Ikolojia. Vinjari [kitabu cha mikakati ya kuboresha mifumo ya ikolojia](#) kupata mawazo.
- Fanya kampeni katika eneo ya kuchukua hatua za kushughulikia uchafuzi wa mazingira kama vile kutengeneza maeneo yenye uchafuzi mdogo au kuboresha usimamizi na utupaji taka; ikijumuisha plastiki, na virutubishi vya shambani.
- Fanya mjadala wa hadhara unaohusisha wadau mbalimbali ili kutambua hatua zenye ufanisi zaidi kuelekea uendeleu wa

mtaa unaoungwa mkono zaidi na kuwasilisha kwa wanaofanya maamuzi.

- Shawishi viongozi wa serikali kuhusiana na sera kali ambazo huathiri mtindo wetu wa maisha, kama vile kuondoa fueli ya visukuku, na kupendelea kuhamia kwa mbinu zisizochafua mazingira, ikijumuisha kutembea, kuendesha baiskeli na kushiriki gari au hatua nyingine mahususi kutegemea sekta.

Jiunge

Jiunge na mpango mpana zaidi wa kushughulikia dharura za sayari ili kukusanya maarifa na rasilimali na kuunda msukumo wa kubadilisha uhusiano kati ya watu na mazingira. Kwa mfano, unaweza:

- Kujiunga na miungano ya mitaa au ya kitaifa ya mashirika yanayotoa wito wa mabadiliko chanya na kushiriki katika mazungumzo na makongamano yanayoitishwa na serikali na mashirika mengine kuhusu mazingira.
- Tazama [Zana za Kupanga Jamii](#) ili upate maelezo zaidi ya jinsi unaweza kufanya mji wako, klabu, shule au kikundi cha kidini kichukue hatua za kuboresha mifumo ya ikolojia.
- Jiunge na [Faith for Earth Initiative](#) ya UNEP ili kufanya kazi pamoja na vikundi vingine vya kidini katika vita dhidi ya uharibifu wa mazingira.
- Jiunge na mpango kama wa [Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu](#)

[Taka ya Bahari](#), [Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Usimamizi wa Virutubishi](#) au mpango wa [Bahari za Kanda](#) ili kusaidia kutambua vyanzo na suluhisho kwa uchafuzi wa bahari.

- Jiunge na maadhimisho ya [Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu](#) ili kuwezesha uboreshaji wa hewa ili kulinda sio afya ya binadamu tu bali pia sayari.
- Jiunge na [kampeni ya Bahari Safi](#) na ukabiliane na uchafuzi wa plastiki.

Ongoza kwa njia inayoweza kuigwa

Shauri shirika lako au jamii ya kidini ili kupunguza athari zake kwa mazingira na kuwahimiza wenzako kupunguza uchafuzi wao wa kibinafsi kwa mazingira. Kwa mfano, unaweza:

- Hamisha akiba ya shirika lako, mpango wa malipo ya uzeeni na ufadhili wa uwekezaji wa kifedha kwa mashirika yanayounga mkono endelevu na hazidhuru tabianchi, afya ya binadamu au bayoanuai.
- Tathmini athari za mazingira za shirika lako au shughuli na majengo ya vikundi, pamoja na maji yako na matumizi yako ya nishati au ununuzi wako wa bidhaa, na kuandaa mpango wenye malengo wazi ya kuzipunguza.
- Toa hotuba au mahubiri ya kidini yanayoeleza umuhimu wa kuchukua hatua kuhusu uendeleu na kushiriki mwongozo huu

halisi na wanachama wako kuwahimiza kupunguza uchafuzi wao binafsi au wa biashara kwa mazingira.

- Fanya utunzaji wa mazingira kuwa sehemu ya kanuni za mwongozo za shirika lako na kuziwasilisha kwa wanachama wako na umma kwa ujumla.
- Kutegemeza mipango ambayo inakuza maisha endelevu, kama kutoa milo yenye afya, ya mimea kwa wafanyakazi wako na jamii wakati wa hafla na maadhimisho, au kuhimiza wafanyakazi wako na jamii kutembea, kuendesha baiskeli na kutumia usafiri wa umma.

Viungo

<https://www.unep.org/about-un-environment/faith-earth-initiative>

www.AnatomyofAction.org



Sayansi na elimu

Hatuwezi kubadilisha jamii na uchumi wetu tusipojua jinsi ya kufanya hivyo. Kizazi kijacho, ambacho kitapata hasara kubwa kutokana na uharibifu wa mazingira, kinahitaji maarifa na zana kwa haraka ili kuleta mabadiliko chanya. Ndiyo maana sayansi na elimu ni muhimu sana katika juhudi zetu za kubadilisha uchumi na jamii zetu.

Uelewaji wetu wa ulimwengu asili na vilevile uwezo wetu wa kiteknolojia unakua kwa kasi, kufungua fursa zaidi na zaidi. Hizi hapa ni baadhi ya hatua ambazo vyuo vikuu, taasisi za utafiti, shule, wanasayansi na walimu wanaweza kuchukua ili kuongeza kasi.

Pia hatua kupitia utafiti

- Tenga rasilimali zaidi za utafiti ili kutengeneza teknolojia mpya za uzalishaji, usambazaji na uhifadhi wa nishati ili kuharakisha mabadiliko ya sekta ya nishati.
- Tafiti kuhusu njia bora zaidi za kusaidia mifumo ya ikolojia kuboreshwa baada ya uharibifu – kuanzia mashamba hadi kwa misitu, mito na bahari.
- Lenga kutengeneza vifaa viwandani vyenye uchafuzi mdogo ambavyo vinaweza kutengenezwa kwa uendelevu, vinavyoweza kutumika kwa muda mrefu, na ni rahisi kuchakata tena au kutengeneza upya.

- Fanyia kazi aina mpya ya mazao na mifugo ambayo inaweza kutusaidia kuongeza uzalishaji wa chakula huku tukitumia ardhi kidogo na kemikali chache zinazosababisha uchafuzi.
- Tumia uwezo wa sayansi ya raia na uhusishe maelfu ya watu katika, kwa mfano, kuchunguza ndege, wadudu, wanyamapori na kuripoti uchafuzi wa mazingira.
- Shirikiana na shule za biashara ili kuandaa mitaala ya kuelimisha wajasiriamali wanaolinda mazingira kuhusu muundo wa biashara usiochafua mazingira
- Shirikiana na waelimishaji na washawishi katika vyombo vya habari na sanaa ili kujumuisha maisha endelevu na ujumbe wa matumaini katika muktadha wetu wa kitamaduni.

Kuza waleta mabadiliko kwa kutumia elimu

- Kuleta uendelevu katika programu za elimu kwa ajili ya vizazi vyote ili waelewe hatari zinazokabili kizazi chao na jinsi tunavyoweza kuleta mabadiliko chanya.
- Pata maelezo zaidi kuhusu [Muundo Endelevu wa UNEP wa Chuo Kikuu Endelevu](#) au angalia [Race to Zero](#) ya Vyuo Vikuu.
- Buni klabu ya mazingira ili wanafunzi waanze kutafuta kwa undani zaidi masuluhisho ya mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa bayoanuai na uchafuzi wa mazingira.

- Fanya hafla ya Siku ya Mazingira Duniani kwa ajili ya wanafunzi wako ambapo watawaandikia viongozi wa serikali za mitaa na kitaifa wakizungumzia mabadiliko ambayo wangependa kuona.
- Chunguza athari za taasisi yako na shughuli zake kwa mazingira na kuandaa mpango, unaojumuisha malengo yanayopimika, ili kuifanya endelevu zaidi.

Ongoza kwa njia inayoweza kuigwa

- Hamisha akiba ya shirika lako, mpango wa malipo ya uzeeni na ufadhili wa uwekezaji wa kifedha kwa mashirika yanayounga mkono endelevu na hazidhuru tabianchi, afya ya binadamu au bayoanuai.
- Angalia [Zana ya Kupanga Jamii](#) ili ujifunze zaidi jinsi ya kufanya shule yako ichukue hatua za kuboresha mifumo ya ikolojia.
- Hakikisha majengo unayofanyia kazi yana vihami ili kuboresha matumizi ya nishati na, inapowezekana, kubadili mhudumu wako wa nishati na yule anayetumia nishati jadidifu.
- Fikiria kujenga shule yako kwa kutumia vifaa vya mtaani na endelevu, kama vile mbao endelevu.
- Wape wafanyakazi na wanafunzi wako lishe bora, yenye afya, ikijumuisha vyakula vya mimea na chagua inayopatikana mtaani, na katika hafla za umma.

- Wachochee na uwatie moyo wafanyakazi wako na wanafunzi kutembea, kuendesha baiskeli na kutumia usafiri wa umma kufika mahali pao pa kusomea au kufanyia kazi.
- Buni fursa za vijana kujumuika na mazingira, kama vile shughuli za michezo ya nje na safari wakiongozwa kugundua mimea na wanyama wa mitaani.

Viungo

<https://ed.ted.com/earth-school>

<https://schools.wwf.ca/> (Living Planet @ School)

<https://natureforall.global/discovery-zone>

<https://en.unesco.org/themes/education-sustainable-development>



Watu binafsi

Kama raia, wafanyakazi, wanafunzi, watumiaji au katika majukumu mengine yoyote, maamuzi yetu ya kibinafsi huathiri jinsi jamii zetu zinavyoathiri mazingira. Pamoja na kufanya maisha yetu ya kibinafsi kuwa endelevu zaidi, kama watu binafsi tunaweza kushinikiza na kuunga mkono mabadiliko ya mazingira ya haraka na makuu kutoka kwa mashirika makubwa kama serikali na biashara.

Usinyamaze

Tetea mabadiliko makubwa ambayo kwa hakika yanabadilisha uhusiano wetu na sayari. Hapa kuna njia kadhaa za kufanya usikike:

- **TETE MABADILIKO** – Unga mkono viongozi walio na ahadi wazi na/au rekodi ya kushughulikia dharura za mazingira ikijumuisha mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa bayoanuai na uchafuzi wa mazingira. Himiza serikali yako ijiunge na muungano wa [kutozalisha gesi chafu](#), kuishi kulingana na au kuongeza [juhuri zao za kuboresha](#) mifumo ya ikolojia na kupatana na [Mkataba wa Paris](#).
- **ANZA MJADALA** – Anzisha ombi, panga mjadala au anza maandamano ili kuhimiza serikali yako ya – kitaifa au mtaa, ikijumuisha ngazi ya jiji – vile vile wafanyabiashara wakubwa kujiunga na muungano wa kutozalisha gesi chafu, kubadilisha usafiri, kuboresha na kutunza mazingira na kusafisha hewa na maji yetu.
- **OMBA HATUA KUCHUKULIWA** – Uliza baraza lako la jiji, mwajiri, shule au chuo kikuu kuweka malengo endelevu, jiunge na

[Muungano wa Kutozalisha Gesi Chafu](#), uunge mkono [Muongo wa UN wa Kuboresha Mifumo ya Ikolojia](#) na ushiriki katika juhudi za kuleta na kufuatilia maendeleo. Kuhimiza, kuweka shinikizo na kuunga mkono serikali yako ya kitaifa na ya mtaa na biashara katika kuchukua hatua za kuboresha ubora wa hewa kwa kushughulikia vyanzo vya uchafuzi wa hewa.

- **KAMPENI** – Ya mipango endelevu ya miji, ikijumuisha kuboresha maeneo yaliyotumika visivyo au yaliyochafuliwa, kujumuisha maeneo safi katika miradi mipya ya ujenzi wa nyumba, na mitandao imara ya usafiri wa umma.
- **SAMBAZA MAARIFA** – Jifunze kwa kina kuhusu sayansi kuhusu suala linalokuhusu wewe na sambaza maarifa yako kwa marafiki, familia na kwa jamii yako kwa jumla, na katika mijadala ya hadhara, ikijumuisha Mitandao ya kijamii
- **JIHUSISHE** – Jiunge na shirika la mtaani ambalo linajiendeleza kwa uendelevu na kuboresha mazingira ikijumuisha kutetea mabadiliko ya kimfumo.

Kwa mifano zaidi ya mabadiliko ya mageuzi ambayo unaweza kutoa wito kwa serikali na wahusika wengine kuharakisha, soma sehemu zingine kwenye mwongozo huu.

Viungo

<https://www.unep.org/explore-topics/climate-action/act-now>

<https://natureforall.global/home>

Fanya maamuzi endelevu

Ifuatayo ni baadhi ya njia nyingi ambazo tunaweza kubadilisha maisha yetu wenyewe. Yakijumlishwa, chaguzi endelevu za kibinafsi zina uwezo wa kuunda upya uchumi wa mitaani na wa kitaifa na kuwezesha mabadiliko chanya.

Pesa

Uwekezaji wa kifedha ni nyenzo kuu mikononi mwa watu binafsi, wanafunzi, vikundi vya kijamii na wafanyakazi. Angalia na uhakikishe kuwa akiba yako ya kibinafsi, mahali pa kazi, mji, shule au shirika la jamii yako, malipo ya uzeeni au vitega uchumi viko na taasisi za kifedha zinazoweka na kufikia viwango vya juu vya uendelevu – hizo ndizo kampuni za siku zijazo! Ikiwa unamiliki, ulirithi au ulinunua nyumba yako mwenyewe au mali nyingine, okoa nishati na pesa kwa muda mrefu kwa kuweka vihami na kufanya mifumo yake ya joto na baridi iwe bora na endelevu iwezekanavyo.

- **MAADILI YA UWEKEZAJI** – Tumia kanuni zako kuongoza uwekezaji na kuzingatia chaguzi za kuwajibika kijamii na kimazingira. Kwa mfano, kuhamisha akaunti yako kwa benki endelevu na kuwekeza kwenye hisa na dhamana iliyotolewa na makampuni ya nishati jadidifu, wazalishaji wa bidhaa zisizochafua mazingira au wachafuzi ambao wanarekebisha kabisa vitendo vyao.
- **KUTOWEKEZA** – kinyume na hapo juu, usiwekeze katika makampuni yenye uchafuzi mkubwa wa mazingira, kama zile zinazohusishwa na ukataji miti, uchafuzi wa maji, fueli ya visukuku, au kutumia rasilimali kupita kiasi.

- **NYUMBA ZENYE NISHATI CHANYA** – Tumia mifumo mizuri ya upashaji joto na baridi ili kuokoa sayari na kupunguza gharama. Kubadilisha mazoea yako pia kunaweza kuleta mabadiliko makubwa, hivyo ongeza au punguza kiwango cha thermostati, ongeza au punguza nguo moja na usipashe au punguza joto tu kwa vyumba vinavyotumika.
- **HIFADHI NISHATI** – Hami nyumba yako na pendekeza vihami katika mahali pako pa kazi, kuweka baridi majira ya joto na joto katika majira ya baridi. Zima taa na vifaa vya kielektroni wakati havitumikia, tumia vifaa vyenye ukadiriaji wa juu wa matumizi mazuri ya nishati nyumbani kwako. Hii itapunguza uchafuzi na kuokoa pesa.

Chakula

Idadi ya watu duniani inapokaribia kufika bilioni 9 ifikapo 2050, uhitaji wa chakula unaongezeka kwa kasi, na hivyo kuongeza shinikizo kwa maliasili za Dunia. Sote tunaweza kusaidia kupunguza athari mbaya kwa mabadiliko madogo katika jinsi tunavyonunua na kutumia chakula. Lishe bora, inayotokana na mimea ni nzuri kwa afya zetu na kwa sayari.

- **TUMIA LISHE BORA** – A [lishe bora](#) ni mlo unaotoa nguvu na virutubishi kutoka kwa makundi mbalimbali ya vyakula. Punguza vyakula vinavyohitaji malighafi zaidi, hasa maji, kuzalisha (nyama hutumia zaidi ya mimea au kunde), au matunda na mboga ambazo haziko katika msimu au zinaagizwa kutoka mbali.
- **TUMIA VYAKULA VYAKO VYOTE** – Nunua tu chakula unachohitaji tumia chote –ukikitupa, unatupa pesa zako mwenyewe! Hifadhi chakula kwa uangalifu ili kuzuia kisiharibike na fanya mabaki yoyote kuwa mbolea.

- **KUZA CHAKULA CHAKO** – Kukuza chakula chako mwenyewe hakuokoi pesa tu. Pia hupunguza usafiri, upakiaji, na uharibifu wa chakula. Kukuza mimea katika bustani yako au kwenye roshani yako inaweza hata kuboresha ustawi wako wa kiakili.

Vitu

Chaguo za wateja ni muhimu katika kuhamia uchumi unaotumia bidhaa tena na tena na endelevu. Kununua bidhaa na huduma zenye kiwango cha chini cha uchafuzi kwa mazingira – na kununua tu bidhaa ambazo unahitaji na unaweza kushiriki na wengine – huboresha biashara zisizochafua mazingira huku wachafuzi wakipungua. Ni njia ya kuwekeza katika mustakabali bora.

- **MBALI NA KUNUNUA** – Fikiria kuhusu kile unachohitaji na punguza kiasi cha vitu unavyonunua – na kutupa. Chagua vitu ambavyo vimeundwa kudumu na ambavyo vinaweza kutumika tena au vitumiwe kwa makusudi mapya. Labda unaweza kupata unachohitaji kati ya vitu vilivyotumika.
- **CHAGUA BIDHAA ZA KIASILI** – Nunua bidhaa zinazotegemeza mifumo ya ikolojia na jamii za mitaa, kama vile mbao endelevu.
- **KUPUNGUZA MITINDO** – Nunua nguo chache na bora zaidi ambazo bado utapenda hata zikizeeka. Epuka mtindo wa haraka ambao hutengenezwa kwa wingi inayodhuru mazingira na viwango vya kazi katika nchi maskini zaidi. Mtindo hujirudiarudia – unda mtindo wako mwenyewe kwa kutumia nguo bora zilizotumika kutoka miongo kadhaa iliyopita!
- **ACHANA NA BIDHAA ZA MATUMIZI YA MARA MOJA** – Achana na bidhaa za kila siku ambazo haziwezi kutumika tena, kama vile vyombo vya plastiki, mifuko ya plastiki, betri na bidhaa za usafi.

Kila mara kuna njia mbadala endelevu! Toa [Ahadi ya Bahari Safi](#) ili kupunguza uchafuzi wako wa plastiki.

Usafiri

Usafiri wa kibinafsi ni mchangiaji mkubwa katika janga la tabianchi. Kusafiri kwa magari yanayotumia petroli na dizeli na kwa ndege kunachangia uzalishaji wa gesi chafuzi katika sekta ya usafiri, hasa katika nchi zenye mapato ya juu. Na usafiri kutumia fueli ya visikuku ni chanzo kikubwa cha uchafuzi wa hewa unaoua mamilioni ya watu kabla ya wakati kila mwaka.

- **FANYA MAZOEZI** – Tembea au endesha baiskeli zaidi ili kupunguza uchafuzi wa magari kwa mazingira na msongamano kwenye barabara huku ukipata hewa safi na kuimarisha siha yako. Kadiri watu wanavyotumia vijia vya baiskeli na vya kutembea, ndivyo serikali zitakavyohitaji kutengeneza upya miundombinu ili kupunguza kutegemea magari.
- **SHIRIKI MBINU YA USAFIRI** – Ikiwa kutembea au kuendesha baiskeli hakufai, chagua usafiri wa umma na wa pamoja badala ya kuendesha gari. Ungana na familia, marafiki na wafanyakazi wenzako kushiriki mbinu ya usafiri – na gharama yoyote ya usafiri wa gari.
- **ACHANA NA NDEGE** – Gundua maeneo ya likizo yaliyo karibu, mifumo ya ikolojia mitaani au umbali unaoweza kusafiri kwa treni, basi na baiskeli.
- **CHAGUA MBINU ISIYOCHAFUA MAZINGIRA** – Chagua mbinu zisizochafua mazingira kama magari ya umeme na fueli isiyochafua mazingira, na kupunguza usafiri wako kwa jumla, kwa mfano kwa kupunguza safari za wikendi za kwenda maeneo ya mitaani. Chukua likizo karibu na nyumbani na epuka usafiri wa ndege.

Burudani

Jinsi tunavyotumia wakati wetu wa mapumziko huathiri sana athari zetu kwa mazingira. Matembezi na likizo zinaweza kuhusisha safari ndefu, zinazochafua - na zenye mafadhaiko. Nyenzo tunazotumia na shughuli tunazoshiriki pia zinatofautiana na rasilimali zinazotumika. Jishughulisha na matukio ambayo yanakufanya kuishi vyema na sayari

- **FURAHIA SAFARI** – Kukaa mtaani kwa matembezi na likizo kunaweza kupunguza kiwango chako cha uchafuzi, kukuokolea pesa na kuruhusu kusafiri polepole zaidi, bila kusumbuliwa na safari ndefu. Ukienda mbali, safiri mara chache lakini kaa muda mrefu zaidi mara nyingi.
- **JIFUNZE JINSI YA KUBORESHA MAZINGIRA** – Tumia muda kwenye mashamba yanayotumia mbolea ya kiasili au ujiunge na [kambi ya kuboresha mfumo wa ikolojia](#) wakati wa safari yako.
- **DADISI** – Kubali maisha ya kujifunza kila mara, kugundua, na udadisi, na kuwa na mtazamo wazi. Kuna njia nyingi endelevu za kuishi maisha mazuri, kwa hivyo tafuta kinachoeleweka na uchukue hatua!
- **FANYA MAAMUZI** – Fikiria kutumia muda zaidi na rasilimali kwenye mambo yanayoongeza thamani kwa maisha yako bila kuacha uchafuzi mkubwa wa mazingira. Inaweza kuwa matukio ya kitamaduni, michezo ya timu, kozi ya kujifunza ujuzi mpya, au kujitolea katika mpango wa kuboresha mfumo wa ikolojia.

Viungo

www.AnatomyofAction.org

<https://breathelife2030.org/challenge/>

<https://www.un.org/en/actnow/>





Picha: Patrick/Pexels



#DuniaMojaTu

KWA HABARI ZAIDI:

<https://www.worldenvironmentday.global/sw>

unep-communication-director@un.org

unep.org

United Nations Avenue, Gigiri, S.L.P 30552, 00100 Nairobi, Kenya



SIKU YA
MAZINGIRA
DUNIANI 2022



Sweden
Sverige